## هَمْزَةُ الْوَصْلِ **Hamzatul-Waswl – Hamza ya kuunganisha:**

Ni hamzah inayotamkwa katika neno na haitamkwi (hutoweka) wakati wa kuunganisha na neno la nyuma yake.

Inaitwa 'Waswl' kwa sababu inaupelekea ulimi kuweza kutamka herufi inayoanzia na herufi yenye sukuwn; na kwa sababu hiyo ndio ikaitwa سُلَّمُ اللِّسَانِ (sullamul-lisaan - ngazi ya ulimi) kwa sababu inaeleweka kuwa maneno ya kiarabu yote hayaanzwi kwa herufi yenye sukuwn [1].

Vipi kuitamka inapounganishwa na neno kabla yake:

قُلِ ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ وَسَلَٰمٌ عَلَىٰ عِبَادِهِ ٱلَّذِينَ ٱصْطَفَىٰٓ

***((Qulil-Hamduli-LLaahi wa salaamun-'alaa 'ibaadihi-lladhiyna-stwafaa))***

Hamzah katika neno ٱلْحَمْدُ na ٱلَّذِينَ na ٱصْطَفَىٰ haitamkwi kwa vile yameungana maneno kabla yake. Au sivyo ingelikuwa ni kutamkwa ifuatavyo ambavyo itakuwa ni makosa kwa sababu maneno yatakuwa yanakatwakatwa:

***((Qul Al-HamduliLLaahi wa salaamun 'alaa 'ibaadhihi alladhiyna astwafaa))***

Vipi kuanzia kutamka هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl)

هَمْزَةُ الْوَصْلِ Hupatikana katika اسم (ism – nomino), فِعْل (fi'l – kitenzi) na herufi حَرْف (harf – herufi) moja tu ambayo ni لامُ التَّعْرِيف (laamut-ta'riyf - ya kibainishi

[1]Waarabu hawaanzi kwa sukuwn na wala hawasimami kwa harakah, hii ni kanuni inayoeleweka katika lugha ya Kiarabu; hii ni kusema kuwa haiwezekani kuanza kutamka neno lenye sukuwn; hivyo basi itapokuwa mwanzo wa neno ipo herufi ya sukuwn, patahitajika hamzah hii ya waswl ili kuweza kulitamka hilo neno..

ال) ; lakini katika kutamkwa kwake, *i'raab* ya هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) hubadilika kwa kuwa inategemea kile kinachokutana nacho hiyo hamzah.

1- هَمْزَةُ الْوَصْلِ فِي الأَسْمَاءِ - **Hamzatul-Waswl katika nomino** (اسم)

Inaweza kuwa katika nomino za kawaida na zisizo za kawaida.

Katika nomino za kawaida kama مَصْدَر (maswdar - asili ya neno) ya kitenzi kilichopita خماسي (khumaasiy – kitenzi chenye herufi tano) na سداسي (sudaasiy – kitenzi chenye herufi sita) hutamkwa kwa kasrah:

| Aayah | Matamshi | Neno |
|---|---|---|
| وَحَرَّمُوا۟ مَا رَزَقَهُمُ ٱللَّهُ ٱفْتِرَآءً عَلَى ٱللَّهِ ۚ [2] | iftiraaaa | ٱفْتِرَآءً |
| إِنَّ فِي ٱخْتِلَٰفِ ٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ [3] | ikhtilaaf | ٱخْتِلَٰفِ |
| وَمَا كَانَ ٱسْتِغْفَارُ إِبْرَٰهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا عَن مَّوْعِدَةٍ وَعَدَهَآ إِيَّاهُ [4] | istighfaar | ٱسْتِغْفَارُ |
| وَلَوْ يُعَجِّلُ ٱللَّهُ لِلنَّاسِ ٱلشَّرَّ ٱسْتِعْجَالَهُم بِٱلْخَيْرِ لَقُضِيَ إِلَيْهِمْ أَجَلُهُمْ ۖ [5] | isti'jaalahum | ٱسْتِعْجَالَهُم |
| وَأَصَرُّوا۟ وَٱسْتَكْبَرُوا۟ ٱسْتِكْبَارًا [6] | istikbaaraa | ٱسْتِكْبَارًا |

[2]Al-An'aam (6: 140)
[3]Yuwnus (10: 6)
[4]At-Tawbah (9: 114)
[5]Yuwnus (10 : 11)
[6]Nuwh (71 : 7)

Katika nomino zisizo za kawaida hutamkwa pia kwa kasrah ikiwa itaanzwa kusomwa yenyewe, nayo imetokea katika maneno saba pekee katika Qur-aan yaliyokuja katika mifumo kadhaa.

| Linapoanza kutamkwa | Matamshi inapoungwa | Aayah | Neno |
|---|---|---|---|
| ibniy | innab-niy<br><br>Bonyeza usikilize | وَنَادَىٰ نُوحٌ رَّبَّهُۥ فَقَالَ رَبِّ إِنَّ ٱبْنِى مِنْ أَهْلِى [7] | ابن |
| ibna | yaa 'Iysab-na Maryam<br><br>Bonyeza usikilize | إِذْ قَالَ ٱلْحَوَارِيُّونَ يَـٰعِيسَى ٱبْنَ مَرْيَمَ [8] | |
| ibnata | wa Maryamab-nata<br><br>Bonyeza usikilize | وَمَرْيَمَ ٱبْنَتَ عِمْرَٰنَ ٱلَّتِىٓ أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا [9] | ابنت |
| ibnatayya | ihdab-natayya<br><br>Bonyeza usikilize | قَالَ إِنِّىٓ أُرِيدُ أَنْ أُنكِحَكَ إِحْدَى ٱبْنَتَىَّ هَـٰتَيْنِ [10] | |
| imri-in | kullum-riin<br><br>Bonyeza usikilize | كُلُّ ٱمْرِىٍٕۭ بِمَا كَسَبَ رَهِينٌ [11] | امرؤ [12] |

---

[7]Huwd (11 : 45)
[8]Al-Maaidah (5: 112)
[9]At-Tahriym (66 : 12)
[10]Al-Qaswasw (28: 27)
[11]At-Twuwr (52: 21)
[12]Neno pekee ambalo هَمْزَةُ الْقَطْعِ (hamzatul-qatw') ya mwisho wa neno inabadilika *i'raab* yake kuwa ima raf'u (dhwammah), jarr (kasrah) au naswb (fat-hah) kutegemea hali yake ya swarf katika kauli.

| | | | |
|---|---|---|---|
| imru-un | inim-ru-un<br><br>Bonyeza usikilize | إِنِ ٱمْرُؤٌا۟ هَلَكَ لَيْسَ لَهُۥ وَلَدٌ [13] | |
| imra-an | abuwkim-raa<br><br>Bonyeza usikilize | مَا كَانَ أَبُوكِ ٱمْرَأَ سَوْءٍ | |
| imra-ata | aamanum-ra-ata<br><br>Bonyeza usikilize | وَضَرَبَ ٱللَّهُ مَثَلًا لِّلَّذِينَ<br>ءَامَنُوا۟ ٱمْرَأَتَ فِرْعَوْنَ [14] | امرأت<br>au<br>امرأة |
| imra-atayni | min duwnihimum-ra-atayni…<br><br>Bonyeza usikilize | وَوَجَدَ مِن دُونِهِمُ ٱمْرَأَتَيْنِ تَذُودَانِ [15] | |
| imra-atun | wa inim-ra-atun<br><br>Bonyeza usikilize | وَإِنِ ٱمْرَأَةٌ خَافَتْ مِنۢ بَعْلِهَا نُشُوزًا | |
| ithnaani | al-waswiyyatith-naani<br><br>Bonyeza usikilize | إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ ٱلْمَوْتُ حِينَ<br>ٱلْوَصِيَّةِ ٱثْنَانِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ [16] | اثنين |

[13]An-Nisaa (5: 176)
[14]At-Tahriym (66: 11)
[15]Al-Qaswasw(28 :23)
[16]Al-Maaidah (5: 106)

| | | | |
|---|---|---|---|
| **ithnayni** | **thaaniyath-nayni**<br>**Bonyeza usikilize** | إِذۡ أَخۡرَجَهُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ ثَانِيَ ٱثۡنَيۡنِ [17] | |
| **ithnataa** | **minhuth-nataa**<br>**Bonyeza usikilize** | فَٱنفَجَرَتۡ مِنۡهُ ٱثۡنَتَا عَشۡرَةَ عَيۡنٗاۖ [18] | اثنتين |
| **ithnatay** | **wa qatw-twa'naahumuth-natay**<br>**Bonyeza usikilize** | وَقَطَّعۡنَٰهُمُ ٱثۡنَتَيۡ عَشۡرَةَ أَسۡبَاطًا أُمَمٗاۚ [19] | |
| **ismuhu** | **mim-ba'-dis-muhuu**<br>**Bonyeza usikilize** | وَمُبَشِّرَۢا بِرَسُولٖ يَأۡتِي مِنۢ بَعۡدِي ٱسۡمُهُۥٓ أَحۡمَدُۖ [20] | اسم |
| **isma** | **sabbihis-ma**<br>**Bonyeza usikilize** | سَبِّحِ ٱسۡمَ رَبِّكَ ٱلۡأَعۡلَى [21] | |

**2- هَمْزَةُ الْوَصْلِ فِي الْحُرُوفِ - Hamzatul-Waswl Katika Herufi**

هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-wasw) Inapotokezea katika herufi ya لاَمُ التَّعْرِيف (laamut-ta'riyf - ya kibainishi ال) hutamkwa kwa fat-hah daima ikiwa msomaji

[17]At-Tawbah (9: 40)
[18]Al-Baqarah (2: 60)
[19]Al-A'raaf (7: 160)
[20]As-Swaff (61: 6)
[21]Al-A'alaa (87: 1)

ataanzia na neno. Ama akiendelea haitotamkwa. Mifano iliyokariri ni katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) :

هُوَ ٱللَّهُ ٱلَّذِى لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْمَلِكُ ٱلْقُدُّوسُ ٱلسَّلَٰمُ ٱلْمُؤْمِنُ ٱلْمُهَيْمِنُ ٱلْعَزِيزُ ٱلْجَبَّارُ
ٱلْمُتَكَبِّرُ ۚ سُبْحَٰنَ ٱللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٢٣﴾ [22]

إِنَّ ٱلْمُسْلِمِينَ وَٱلْمُسْلِمَٰتِ وَٱلْمُؤْمِنِينَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتِ وَٱلْقَٰنِتِينَ وَٱلْقَٰنِتَٰتِ وَٱلصَّٰدِقِينَ
وَٱلصَّٰدِقَٰتِ وَٱلصَّٰبِرِينَ وَٱلصَّٰبِرَٰتِ وَٱلْخَٰشِعِينَ وَٱلْخَٰشِعَٰتِ وَٱلْمُتَصَدِّقِينَ وَٱلْمُتَصَدِّقَٰتِ
وَٱلصَّٰٓئِمِينَ وَٱلصَّٰٓئِمَٰتِ وَٱلْحَٰفِظِينَ فُرُوجَهُمْ وَٱلْحَٰفِظَٰتِ وَٱلذَّٰكِرِينَ ٱللَّهَ كَثِيرًا
وَٱلذَّٰكِرَٰتِ أَعَدَّ ٱللَّهُ لَهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٥﴾ [23]

**Tanbihi:**

Kuingiza لامُ التَّعْرِيف (laamut-ta'riyf - ya kibainishi ال) katika neno lililo na هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl), haiondoki hukmu yake. Hivyo basi huanziwa kwa أَلْ. Ama هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) ya neno hutoweka kwa maana haitamkwi tena kwa sababu limekuwa katikati ya neno. Mfano ni neno la الإِسم katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

وَلَا تَلْمِزُوٓا۟ أَنفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا۟ بِٱلْأَلْقَٰبِ ۖ بِئْسَ ٱلِٱسْمُ ٱلْفُسُوقُ بَعْدَ ٱلْإِيمَٰنِ ۚ [24]

Ikibidi msomaji asimame katika neno la nyuma yake kama vile الْوَقْفُ الإِخْتِباري (Kisimamo cha mtihani), neno hilo litaanziwa katika hali mbili zifuatazo:

---

[22] Al-Hashr (59: 23)
[23] Al-Ahzaab (33: 35)
[24] Al-Hujuraat (49: 11)

i. Kuanzia kwa hamzah ya fat-hah أَلِسْمُ (alismu)

ii. Kuondosha هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) na kuanzia kwa لِ ya kasrah لِسْمُ (lismu).

**3- هَمْزَةُ الْوَصْلِ فِي الأَفْعَالِ - Hamzatul Waswl Katika Kitenzi:**

هَمْزَةُ الْوَصْلِ (Hamzatul-waswl) inapokuwa katika neno pekee la kitenzi hutamkwa ima kwa kasrah au kwa dhwammah kwa kutegemea *i'raab* ya herufi ya tatu katika neno. Ikiwa *i'raab* katika herufi ya tatu kuanzia kwenye هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) ina fat-hah au kasrah, basi هَمْزَةُ الْوَصْلِ (hamzatul-waswl) hutamkwa kwa kasrah. Ikiwa ina dhwammah, hutamkwa kwa dhwammah.

| Dhwammah Katika Herufi Ya Tatu | | Kasrah Katika Herufi Ya Tatu | | Fat-hah Katika Herufi Ya Tatu | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Matamshi** | **Neno** | **Matamshi** | **Neno** | **Matamshi** | **Neno** |
| **ushdud** | ٱشْدُدْ | **ihdinaa** | ٱهْدِنَا | iqtarabati | ٱقْتَرَبَتِ |
| **uskun** | ٱسْكُنْ | **idhwrib** | ٱضْرِبْ | intwaliquw | ٱنطَلِقُوٓاْ |
| **ubtuliya** | ٱبْتُلِىَ | **infiruu** | ٱنفِرُواْ | istaghfir | ٱسْتَغْفِرْ |
| **u'buduw** | ٱعْبُدُواْ | **iswbir** | ٱصْبِرْ | idh-hab | ٱذْهَبْ |
| **usjuduw** | ٱسْجُدُواْ | **ikshif** | ٱكْشِفْ | irtadhwaa | ٱرْتَضَىٰ |

Isipokuwa: Maneno matano pekee katika Qur-aan ya vitenzi vya kuamuru (أَمْر) ambavyo vimo katika minyambuliko mbali mbali. Hivi japokuwa herufi ya tatu ni dhwammah, lakini yanapaswa kutamkwa kwa kasrah inapoanziwa. Hii ni kwa sababu *i'raab* ya dhwammah katika herufi ya tatu siyo ya asili bali inatokana na sababu ya uwingi (جمع) wa kuamuru.

| Linapoanza kutamkwa | Linapoungwa | Aayah |
|---|---|---|
| **iqdhwuw** | **thummaq-dhwuw...** <br> Bonyeza usikilize | ثُمَّ ٱقْضُوٓا۟ إِلَىَّ وَلَا تُنظِرُونِ [25] |
| **imdhwuw** | **wamdhwuw...** <br> Bonyeza usikilize | وَٱمْضُوا۟ حَيْثُ تُؤْمَرُونَ [26] |
| **ibnuw** | **faqaalub-nuw...** <br> Bonyeza usikilize | فَقَالُوا۟ ٱبْنُوا۟ عَلَيْهِم بُنْيَـٰنًا ۖ [27] |

[25]Yuwnus (10: 71)
[26]Al-Hijr (15: 65)
[27]Al-Kahf (18: 21)

| | | |
|---|---|---|
| imshuw | ...animshuw...<br><br>Bonyeza usikilize | وَٱنطَلَقَ ٱلْمَلَأُ مِنْهُمْ أَنِ ٱمْشُوا۟<br>وَٱصْبِرُوا۟ عَلَىٰٓ ءَالِهَتِكُمْ ۖ [28] |
| iytuwniy<br><br><br><br>iytuw | ...fis-samawaati (+ sukuwn) tuwniy...<br><br>Bonyeza usikilize<br><br><br>...thumma (+ sukuwn) tuw...<br><br>Bonyeza usikilize | أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ ۖ ٱئْتُونِى<br>بِكِتَٰبٍ مِّن قَبْلِ هَٰذَآ [29]<br><br><br>فَأَجْمِعُوا۟ كَيْدَكُمْ ثُمَّ ٱئْتُوا۟ صَفًّا ۚ<br>[30] |

[28]Swaad (38: 6)
[29]Al-Ahqaaf (46: 6)
[30]Twaaha (20: 64)